



Karibu kwenye Huduma ya Watoto Wageni (Care for Newcomer Children – CNC)

*Karibu kwenye mpango
wetu wa CNC!*

*Ili kumsaidia mtoto wako
kuhisi salama, na kumruhusu
kusoma bila kuwa na
wasiwasi, ni muhimu uchukue
muda kiasi kujua mpango na
wahudumu wetu.*

*Wakati mwingine watoto
hulia, kuhisi wamepotea au
kuonyesha hisia kali wakati
wazazi wao wanapotoka kwa
mara ya kwanza. Wasiwasi
huu wa kutenganishwa ni
wa kawaida—hasa ikiwa ni
mara ya kwanza mtoto wako
kuwa katika huduma ya
kundi. Ili kuwasaidia nyinyi
nyote wakati huu, tuna dhibiti
utenganisho wa kwanza
kwa makini kwa kutumia
utenganisho wa polepole.*

Je, utenganisho wa polepole ni nini?

Utenganisho wa polepole humaanisha kuongeza urefu wa utenganisho kati ya mzazi na mtoto anapoendelea kuzoea kuwa katika mpango huu. Inahusisha kushirikisha wahudumu wa mpango na kumwandaa mtoto wako mapema kwa utenganisho wa kwanza.

Utenganisho wa polepole:

- huheshimu mahitaji ya watoto,
- humsaidia mtoto wako kuhisi salama,
- huunga mkono mpito rahisi katika mpango wetu, na
- huweka mpangilio wa kufanikiwa kutenganisha na mahusiano mema kadri mtoto anavyoendelea kukua.

Watoto ambao hupitia kiwewe wakitenganishwa kwa mara ya kwanza huchukua muda mrefu zaidi kutulia katika mpango huu, kwa hivyo tafadhali jiandae kubakia na mtoto wako kama inavyohitajika. Kila mtoto ni tofauti, lakini ni muhimu kutoharakisha mchakato huu.

Jinsi gani hufanya kazi?

Kabla ya kuanza darasa:

- Ikiwezekana, tembelea mpango wetu na mtoto wako.
- Ongea kwa kawaida na wahudumu kuhusu mtoto wako, mpango huu na jinsi wanavyopanga utenganisho huu kwa kawaida. Hii humsaidia mtoto wako kuwaona wahudumu kama watu salama na wanaoweza kuaminika.
- Ikiwezekana, muonyeshe mtoto wako mahali darasa lake litakuwa.

Siku chache za kwanza za mtoto wako

- Jaribu kuwa mtulivu na mwenye matumaini.
- Nenda kwenye eneo ambalo unafikiria mtoto wako atafurahia zaidi na uwaeleze wahudumu kile ambacho mtoto wako anapenda kucheza nacho.
- Lenga zaidi mtoto wako. Zungumza nae, mwonyeshe mwanasesere na cheza nae.
- Kuwa macho kwa maeneo mengine yoyote ambayo wanaonyesha wanavutiwa na ufuate maelekezo yao.
- Tazama ishara kutoka kwa wahudumu.
- Himiza mtoto wako kucheza na watoto wengine au na wahudumu akiwa tayari. Ikiwa mtoto wako haonekani kuwa tayari, ni sawa kusubiri kwa muda zaidi kidogo.

MWONGOZO WA WAZAZI WA UTENGANISHO WA POLEPOLE

- Wakati mtoto wako anaweza kucheza kivyake au na wengine, hii ni ishara nzuri kwamba yupo tayari kujaribu kujitenga kwa mara ya kwanza! Jaribu kuchukua hatua moja nyuma na utazame.
- Ikiwa mtoto wako atakufuata mara moja na aonekane kutaka uwe karibu, huenda hayuko tayari.
- Utenganisho kamili unaweza kuchukua muda mrefu kwa watoto ambao wamepitia uhasama na kiwewe.

Utenganisho wa kwanza

Wakati wewe na wahudumu mnaona kwamba mtoto wako anacheza vizuri na anaonekana yupo sawa, unaweza kuanza kutoka kwenye mpango huu kwa vipindi vifupi.

- Mwambie mtoto wako unaenda msalani na kwamba utarejea baada ya dakika mbili.
- Usiwahi kutoka chumbani bila kuwafahamisha wahudumu kwamba unaenda.
- Nenda msalani na uhakikishe umerejea kama ulivyosema.
- Ikiwa utenganisho huu wa kwanza unampa mtoto wako kiwewe, huenda hayuko tayari.

Baada ya utenganisho wa kwanza kwenda vizuri, basi uko tayari kujaribu utenganisho wa pili ambao unachukua muda mrefu zaidi (dakika 5-15). Na kisha wa tatu, na hata utenganisho wa muda mrefu zaidi (dakika 10-20).

Utenganisho huu wa muda mfupi huleta imani kwa mtoto wako na humsaidia kuelewa kwamba daima utarudi. Kwa kila utenganisho, hakikisha:

- Umekuwa thabiti.
- Mweleze mtoto wako kwamba unaenda. Kwenda bila kusema huvunja imani na kutafanya iwe vigumu zaidi kujitenga baadaye.
- Hakikisha kwaheri yako ni fupi kama iwezekanavyo na uwe na mhadumu mmoja/anayemtambua hapo ili kumsaidia mtoto wako unapoondoka.

- Zingatia mambo mazuri unaporejea. Jaribu kumuuliza mtoto wako kuhusu ni mwanasesere gani alizochezea au alichokipenda zaidi.

Mtoto wako anapoweza kudhibiti utenganisho huu mfupi bila kukerwa sana, yupo tayari kwa wewe kuondoka! Unapoanza kumwacha mtoto wako kwa mara ya kwanza kwa kipindi kizima cha mpango huu, jaribu kuwa mmoja wa watu wa kwanza wa kuja kumchukua ili kushinikiza dhana kwamba daima utakuwa ukirejea.

Je, itakuwaje ikiwa mtoto wangu atakasirika?

Ikiwa bado mtoto wako ana matatizo, jaribu usiwe na wasiwasi. Huenda ukahitaji kuchukua muda zaidi na mtoto wako katika mpango huu ili kumsaidia kuhisi salama na sawa. Kuleta mwanasesere au blanketi, au kuacha skafu au sweta kunaweza pia kumsaidia mtoto wako kuhisi vizuri zaidi.

Wahudumu wa mpango wamesaidia familia nyingi katika mchakato huu na wako hapo kukuongoza na kukusaidia.



KUUNGA MKONO HUDUMA NA MAKAZI YA
WATOTO WADOGO WAHAMIAJI

Kwa vyanzo saidizi zaidi vya wazazi, tembelea:
www.cmascanada.ca



Care for
Newcomer
Children